

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: +255 26 2321607
Nukushi: +255 26 2322116
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

TANGAZO LA KUITWA KAZINI

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inapenda kuwataarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali za kada za afya waliowasilisha maombi katika kipindi cha mwezi wa April, 2023 kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi umekamilika kwa awamu ya tatu. Awamu hii ni kwa ajili ya kujaza nafasi wazi za Watumishi waliokosa ajira awamu zote 2 za awali, Ikumbukwe kuwa Ajira hizi ni za Mkataba ya miaka 2, hivyo wataalamu wote watakojiriwa katika awamu hii wataingia mikataba na Wakurugenzi wa Halmashauri husika.

Mwezi Aprili, 2023 Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipata kibali cha ajira ya watumishi **8,070** wa kada mbalimbali za Afya. Nafasi ambazo zilipata waombaji wa kutosha na kupelekea kubaki kwa baadhi ya waombaji wenye sifa katika kanzi data ya OR TAMISEMI, kutokana na maombi kuzidi idadi ya kibali.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imefanikiwa kutumia kanzi data ya waombaji wenye sifa waliokuwa wamebaki katika mfumo na kuwapangia vituo vya kazi watumishi **275** katika Halmashauri mbalimbali. Ieleweke kwamba ajira hizi ni za Mkataba kati ya Halmashauri husika na mtaalamu husika. Mkataba huu utasimamiwa na OR TAMISEMI wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto yaani **Tanzania Martenity and Child Health Investment program (TMCHIP)** unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Gharama za malipo ya mishahara zitazingatia taratibu za ajira Serikalini.

Waombaji wote waliopata nafasi wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- i) Kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha, waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi ndani ya siku kumi na nne (14) nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.
- ii) Kuwasilisha Vyeti Halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaaluma kwa ajili ya kuhakikiwa na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira.
- iii) Waombaji waliopata nafasi za ajira watakaoripoti bila ya kuwa na Vyeti Halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Kidato Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaaluma hawatapokelewa.
- iv) Waombaji waliopata nafasi za ajira wanajulishwa kuwa hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha vituo vya kazi walivyopangiwa.

Waombaji wote ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili, watambue kuwa hawakupata nafasi hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwapokea, kuhakiki vyeti, Kuandaa na kuingia Mikataba ya ajira na wataalamu waliopangwa na kuwafanyia mafunzo elekezi (Induction Course) kabla ya kuwapangia vituo vya kazi.

Orodha ya majina ya waombaji waliopangiwa vituo vya kazi inapatikana kupitia tovuti ya OR-TAMISEMI www.tamisemi.go.tz.

Limetolewa na:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali – Mtumba,
S.L.P. 1923,
DODOMA.

26 Januari, 2024